

# Matatizo

Matozi yachuruzika, hali twasikitikia,  
Moyoni nimetamauka, imani metuishia,  
Kokote kumekauka, majanga kututishia  
Maji yameadimika, ukame metuzidia.

Matatizo kwa hakika, njaa imetuvamia,  
Hakuna liyeokoka, sote machozi twalia,  
Magonjwa yametufika, daktari kupuuzia,  
Tumejawa na mashaka, Rabana twakulilia.

Vyuoni bila mashaka, wahadhiri walilia,  
Elimu meathirika, wanafunzi wahofia,  
Migomo kazi kushika, hakuna wa kusikia,  
Masomo yamekatika, wanafunzi wamelipia.

*Josphat Cheruiyot,  
Chuo kikuu cha Seku,  
Kitui.*